**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

# TAARIFA YA MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB),WAZIRI WA UCHUKUZI KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU HATUA ZA SERIKALI KUBORESHA USAFIRI WA WANAFUNZI KATIKA MAENEO YA MIJINI

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KAZI NA UTU…TUNASONGA MBELE**

**Ndugu Wanahabari,**

Nimeona *video clip* kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii ambapo binti aliyejitambulisha kwa jina la Mariana Eric Mirindima ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza, Shule ya Sekondari Jangwani akiwasilisha barua yake iliyoeleza changamoto wanazokutana nazo wanafunzi wanaotumia usafiri wa mabasi ya mijini, maarufu kama daladala.

Katika barua yake, Mwanafunzi Mariana ameeleza kwamba makondakta wamekuwa wakigoma kuwabeba wanafunzi kwa kisingizio cha kibiashara wakidai kuwa wanafunzi hawalipi nauli kamili. Kutokana na hali hiyo, wanafunzi wanalazimika kusimama barabarani kwa muda mrefu wakisubiri usafiri, wanachelewa kufika shuleni, na wakati mwingine

wanashindwa kabisa kufika shuleni. Hali hii inawatia hofu wanafunzi, inawachosha, na inaathiri masomo yao, pamoja na usalama wao kama watoto. Alieleza pia kuwa wanafunzi wanategemea sana daladala kama njia yao kuu ya usafiri, hivyo wanapoachwa njiani au kunyimwa huduma wanakuwa kwenye mazingira hatarishi, na kunyimwa haki yao ya msingi ya kupata elimu kwa usalama.

Hivyo, mwanafunzi Mariana akaomba, kwa niaba ya wanafunzi wengine, Wizara yangu ichukue hatua stahiki dhidi ya vitendo wanavyofanyiwa wanafunzi na watoa huduma za daladala (Wamiliki, Madereva na Makondakta). Kisha akamalizia kwa kusema anawasilisha barua hiyo akiwa na matumaini makubwa kwamba sauti ya wanafunzi itasikilizwa na itafanyiwa kazi.

**Ndugu Wanahabari,**

Kwanza, ninamshukuru mwanafunzi huyo na mzazi wake aliyesimamia kwa ujasiri uamuzi huu wa kupaza sauti na kutoa mrejesho kuhusu changamoto hii kupitia mitandao ya kijamii. Kwa kufanya hivyo, kijana huyu na mzazi wake wametimiza wajibu wao wa msingi wa kuipa Serikali na Mamlaka zote husika mrejesho unaopaswa kufanyiwa kazi. Na kwa hakika sauti ya wanafunzi imesikilizwa na itafanyiwa kazi.

**Ndugu Wanahabari,**

Serikali imetoa fursa kwa sekta binafsi kuwa ni watoa huduma za usafiri wa abiria baina ya miji, mijini na vijijini, ikiwa ni pamoja na Daladala zinazotoa huduma mijini. Ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa huduma hizi zinaimarika kila wakati kupitia jukumu walilopewa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kisheria. Serikali itaendelea **kuchukua hatua**

**stahiki dhidi ya watu wote wanaokiuka taratibu na kanuni za usafiri**, bila kujali nafasi zao.

Aidha, katika kukabiliana na changamoto za usafiri wa abiria wakiwemo wanafunzi, Katika kuboresha usafiri wa wanafunzi mijini, Serikali imeweka mipango na mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) **kuanzisha huduma za mabasi maalumu yaendayo haraka kwa ajili ya wanafunzi**, hususan katika nyakati za asubuhi na jioni, ili kuhakikisha wanafunzi wanafika shuleni na kurejea majumbani kwa usalama na kwa wakati;

(ii) **kutenga mabehewa maalumu kwa ajili ya wanafunzi kwenye treni za mijini (Dar es Salaam)**, hatua inayolenga kupunguza msongamano, kuongeza usalama na kutoa unafuu wa usafiri kwa wanafunzi wanaotumia treni za mijini;

(iii) kurasimisha na kusimamia **utozaji wa nauli maalumu ya Shilingi 200 kwa wanafunzi katika mabasi yaendayo haraka na daladala**, kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizowekwa. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata huduma hizi kwa gharama nafuu; na

(iv) Kutekeleza Sheria na Kanuni za **Kuthibitisha Madereva na Kusajili Wahudumu (Makondakta)** wa vyombo vya usafiri wa Umma – Mabasi na Treni

Hatua zote hizi zinalenga kutekeleza **malengo ya Serikali ya kuboresha huduma za kijamii, hususan huduma za wanafunzi katika vyombo vya usafiri**, ili kuwawezesha kupata elimu katika mazingira rafiki na yenye staha.

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kuhakikisha utekelezaji mzuri wa hatua hizi, pamoja na kujibu changamoto zilizowasilishwa na mwanafunzi Mariana, ninaigiza **Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA)** kutekeleza yafuatayo:

1. Kuhakikisha zoezi la **kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu (makondakta) kwenye mabasi linafanywa kwa kasi katika miji yote Nchini**, na kutoa adhabu kali kwa mujibu wa Sheria kwa madereva na makondakta watakaobainika kuwanyanyasa wanafunzi;
2. kuimarisha udhibiti **wa nauli maalumu za wanafunzi, staha ya huduma na usalama wao kwa wakati wote;**
3. **Kuendelea kutoa elimu kwa watoa huduma, na watumia huduma wajue haki na wajibu wa kila mmoja;**
4. **Kuhakikisha Treni za Abiria, Daladala zote Nchini pamoja na Mabasi yaendayo Mikoani na Nchi jirani zimeandikwa namba za bure ili abiria waweze kupiga LATRA 0800 11 00 19 na 0800 11 00 20**; na
5. **Kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na wa kushtukiza kwenye vituo vya daladala hasa nyakati za asubuhi na jioni kuhakikisha wanafunzi wanapata usafiri**.

**Ndugu Wanahabari,**

Mwisho, niwaombe Watanzania, na abiria kwa ujumla, tushirikiane kuwatetea wanafunzi wanaponyanyaswa na mtu yeyote. M**naweza kutuma ushahidi wa picha au sauti kwa namba ya LATRA WhatsApp 0681 300 800**. Aidha, Serikali inaendelea kusisitiza ushirikiano wa wadau wote ili kujenga mfumo wa usafiri wa umma unaolinda haki, usalama na ustawi wa wanafunzi na watu wote nchini.

Aidha, nitoe rai tena kwa wamiliki wa Daladala kuwakumbusha watumishi wao kuzingatia Sheria na Kanuni wanapotoa huduma za usafiri kwa wanafunzi ili kujiepusha na hatua zitakazochukuliwa dhidi yao pale wanapovunja Sheria husika.

***Asanteni kwa kunisikiliza.***

**Prof. Makame M. Mbarawa (Mb)**

**WAZIRI WA UCHUKUZI**

**DODOMA**

**04/02/2026**